TANGAZO LA SERIKALI NA. 391 la tarehe 17/05/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU NA HUDUMA YA HALMASHAURI YA MJI WA HANDENI YA MWAKA 2024

Jina

TS Na 367 la Mwaka 2019

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2019 ambayo katika marekebisho haya itarejewa kama "Sheria Ndogo Kuu"

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kanuni ya 4 kwa kufuta kanuni hiyo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Ushuru wa huduma

4. Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwa mlipa ushuru kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu ya mauzo ya bidhaa au huduma zinazotolewa katika eneo la Halmashauri baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa.".

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Handeni imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji uliofanyika tarehe 07 Mwezi Februari Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya;

MARYAM A. UKWAJU
*Mkugenzi wa Halmashauri*
*Halmashauri ya mji Handeni*

MUSSA A. MKOMBATI
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Mji wa Handeni*

NAKUBALI,

/

L.S

Dodoma,
9 Disemba 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*waziri wa nchi – ofisi ya rais*
*(tawala za mikoa na serikali za mitaa)*